

## **Minyiri ya Utumwa-Lugha na Mtanziko wa Fikra za Kikoloni miongoni mwa Waafrika**

*Aldin Kai. Mutembei<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Maana ya utumwa imekuwa sehemu mojawapo ya mada katika mijadala ya wanazuoni hasa baada ya mwaka 1926. Mpaka mwaka 2012, bado kulikuwa na mjadala wa kisheria kuhusu maana ya utumwa. Mijadala hii haikuangalia sana suala la lugha kama nyenzo yenye kuingiza dhana ya kipekee katika maana ya utumwa. Hata hivyo, ni wazi kuwa wakati wa utumwa wa Waarabu, lugha ilitumika kuufanikisha utumwa. Lugha iliubeba utumwa. Wakati wa ukoloni mkongwe, lugha za kikoloni zilijenga matabaka ya kitumwa. Minyiri ya utumwa-lugha ikajiviringa na kuwavunganiza watumwa kifikra na kuwafanya wajikane. Wakati huu wa ukoloni mamboleo, utumwa-lugha umeifanya fikra ya aliyetawaliwa kushikwa na minyiri ya kikoloni kiasi cha kujikuta katika mtanziko: alikotoka hakujui, na kama kuna aendako, hakufahamu. Makala hii ikiongozwa na mawazo ya Frantz Fanon kuhusu lugha (2008), imetumia dhana ya utumwa-lugha kujadili jinsi lugha za watawala wa kikoloni barani Afrika zinavyotokeza utumwa wa kifikra, ambao hatimaye unaharibu misingi mikuu ya kuwapo kwa Mwafrika. Kupitia utumwa-lugha, Waafrika wameachwa katika mtanziko mkubwa wenye mivutano ya ndani inayojibadilisha kuwa minyiri isiyoweza kukatwa na kung'olewa bila ya kuwa na mapinduzi ya kifikra.

### **1.0 Utangulizi**

Makala hii inajadili dhana ya utumwa unaopitia katika lugha. Ingawa itachukua mkabala wa kihistoria kuangalia dhana ya utumwa, itajikita zaidi kufafanua dhana ambayo tunairejelea hapa kuwa ni utumwa-lugha. Dhana hii imekuwapo tangu wakati wa utumwa mkongwe hadi utumwa mamboleo, lakini inafikirisha kuwa katika ujumla wake, suala hili halikuangaliwa kwa kina na wataalamu waliotafiti kuhusu utumwa.

Utumwa-lugha unajadiliwa katika muktadha wa Afrika ambako lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispaniola zimejenga matabaka na kuchukuliwa kuwa za hadhi ya juu (Lodhi, 1993; Mberia, 2015). Wakati huohuo, lugha za asili

---

<sup>1</sup> Profesa, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania  
Barua pepe: [kaimutembei@gmail.com](mailto:kaimutembei@gmail.com)

zikibezwa, kudharauliwa na kuchukuliwa kuwa hazina nafasi katika maisha ya Waafrika (Mabe, 2020). Mwafrika aliyebanwa katikati ya silisila za kitumwa

anajikuta akiwa amenyang'anywa lugha yake ya asili. Kwa kunyang'anywa huku, Mwafrika amepoteza, maarifa, ujuzi, falsafa na thamani ya kuwapo kwake kama Mwafrika. Mawazo ya Frantz Fanon kuhusu lugha (2008) yameongoza mjadala katika makala hii tunapojadili kiunzi cha utumwa-lugha.

Fanon anatuonesha kuwa Mwafrika aliyetawaliwa, hupigiwa makofi ya kejeli na wale waliomtawala pale anapoongea lugha ya mtawala ambayo ina makosa, lakini anaonesha jitihada za kuiongea na huku akiihusudu. Katika Afrika Mashariki, na labda hii ni sawa kwa Afrika yote, mwongaji wa lugha hii huwa na lugha ambayo si sahihi katika sarufi. Ni lugha iliyopoteza usahihi wake, na kama ni Kiingereza inakubalika kuwa ni Kiingereza cha Afrika Magharibi, au cha Afrika Mashariki (Nketia, 1968; Egbonu, 2024). Au kama ni Kifaransa au Kireno, ni kile kilichochanganywa matamshi na msamiati wa asili. Waafrika waongaji wa lugha hizo za watawala wao huwa watumwa wa lugha hizo ambazo huwaondoa katika asili na kuwapeleka mbali katika utumwa wa lugha. Waongaji-watumwa hao hujikuta katika utumwa ambapo wamejiteka wenyewe na kujifungia utumwani; na daima hutegemea kufunguliwa na wenye asili ya lugha hizo, ama kwa kusahihishwa au kusoma zaidi maandishi yao ambayo huja na utamaduni wa lugha hizo za kigeni.

Mwafrika anapoongea lugha hizo za kikoloni, kama asemavyo Fanon (2008), anakuwa kama mtumwa aliyepanda hadhi, akaruhusiwa kuwa na hulka ya bwana wake. Tena, katika hali hiyo ya mtumwa, kuongea lugha ya bwana wake ni kama kwamba mtumwa huyo ameruhusiwa na bwana wake kukaa na kula pamoja na bwana wake mezani kama njia ya kumpa hadhi. Maneno mapya yanayoandikwa ndivyo sivyoyote, sarufi, sentensi na matamshi yasiyokuwa sahihi (Balfour, 2002; Msakha, 2024; Majola, 2024) hupokelewa na bwana mwenye lugha ili kumfanya mtumwa ajisikie kuwa na hadhi ya bwana wake. Katika hali hii, bwana mwenye lugha yake huhakikisha, kwa upande mmoja, anapenyeza taratibu, mila, desturi na utashi wake kwa mtumwa wake. Kwa upande mwingine, anaondoa na kuzuia yale yote yaliyomfanya mtumwa wake ajione mtu au binadamu. Hali hii ya makosa katika lugha inaelezwa na Msakha (2024) kuwa ni kutoka katika 'makosa,' na kuonwa kuwa ni 'aina tofauti' (2024: 26-27); na kwa njia hii, bwana humbadilisha mtumwa kuwa mwanasesere asiyeweza kufanya chochote bila ya kuambiwa au kuelekezwa na bwana wake. Katika kubadilika huku, bwana mwenye watumwa huwa kama mwenye kuwaeleza na kuwatia moyo watumwa wake: "Jitahidi, bado kidogo utafanana na mimi, utakuwa kama mimi". Kwa uaminifu mkubwa mtumwa hujitahidi ili akifanikiwa apewe tuzo kuwa umekaribia kuwa kama bwana wake, Mzungu. Katika hali hii ya mawazo ya kitumwa, Fanon anasema:

Baada ya kuwa mtumwa wa mtu mweupe, sasa mtu mweusi anajiweka utumwani mwenyewe. Kwa kila maana ya neno, mtu mweusi ni mwathirika wa ustaarabu wa mtu mweupe (Fanon, 2008:148).

Kutoka katika kuelekezwa na bwana wake, mtumwa anafikia kiwango cha kuibakiza utumwani fikra yake mwenyewe, na kuionea fahari hali hiyo. Hali hii

inafanywa kupitia katika utumwa-lugha. Mawazo haya ya utumwa-lugha ndiyo yanayojenga mjadala katika makala hii. Makala inajadili jinsi ambavyo lugha za watawala wa kikoloni barani Afrika zinatokeza utumwa wa kifikra, utumwa ambao hatimaye unaharibu misingi mikuu ya kuwako kwa Mwafrika. *Utumwa-lugha* unapoteza maarifa ya asili yaliyomo katika lugha za asili, ujuzi unaobebwa na lugha za asili, na utamaduni na thamani ya utu wa Mwafrika anayejiweka utumwani. Kupitia utumwa-lugha, Waafrika wamejikuta wanaunda sera, sheria na kanuni za kulinda utumwa huu kwa kisingizio cha kushiriki katika maendeleo ya dunia, au kama wengine wasemavyo kutokuachwa na wakati na mabadiliko katika utandawazi. Sera, sheria na kanuni nyingi zinazohusu lugha katika nchi za Afrika, zimeziacha nchi hizo katika mtanziko mkubwa wenye mivutano ya ndani ya kifikra, inayojibadilisha kuwa minyiri isiyoweza kukatwa na kung'olewa bila ya kuwa na mapinduzi ya kifikra. Kuhusu Waafrika wa aina hii, Fanon anaeleza:

Mtu mweusi ni mtumwa kwa kujidunisha mwenyewe, mtu mweupe ni mtumwa kwa kuuvaa ukuu wake, hawa wote wanatenda kulingana na mfumo wa neva unakowaelekeza katika utumwa walionao (Fanon, 2008: xxvii).

Ingawa hoja ya Fanon inachipukia katika uchambuzi wa saikolojia na akili ya binadamu, lakini ndivyo ilivyo katika ulimwengu halisi wa maisha ya watawaliwa. Kwa waliotawaliwa na Waingereza, mtu asipofahamu Kiingereza basi ni mjinga, mbumbumbu, na hana akili (Conboy, 1990). Lakini akiwapo mtu ambaye hakutawaliwa na ikiwa hajui pia Kiingereza, anaangaliwa kwa heshima na staha kwa namna anavyoitumia lugha yake ya asili. Kiingereza (kama Kifaransa na Kireno) kimewaweka Waafrika katika mtanziko wa kifikra, fikra za kitumwa na kutokujiamini. Ukweli huu unaweza pia kuangaliwa kwa namna nyingine. Akiwapo Mfaransa katika jamii za Kiafrika na akawa hawezi kuongea lugha ya jamii aliyomo, anaangaliwa kwa hali au fikra ya kutaka kusaidiwa. Akiiongea lugha ya wenyeji kwa makosa, anashangiliwa na wenye lugha kwa jinsi makosa ayafanyayo yanavyoonwa kuwa ni makosa ya kistaarabu. Ni makosa “yanayovumilika” bila kuingiza hisia za ujuzi wa mambo au ujinga wa kutokujua. Mwenye lugha yake ya asili anajitahidi kumwonesha bwana huyo kuwa kushindwa kwake kuongea lugha ya asili ni kwa vile lugha hiyo ni duni. Ni lugha ambayo mtu mstaarabu na mwenye hadhi kama yake hawezi kushindwa kuiongea. Mtu mwenye mawazo kama haya ni mtumwa ambaye hawezi kujiamini mbele ya bwana wake na mawakala wake. Fanon anamwangaalia hivi mtu wa aina hiyo:

Kwa hivyo, kwa haraka, mtu mweusi anaingia katika mtanziko umleteao shida: weusi wake huonekaneje kupitia katika lugha na katika mazungumzo ambapo weusi wenyewe kwa ubora wake ni alama ya kutokuwepo, au mbaya zaidi ni utimilifu wa kupotea? Hata hivyo, tatizo, haliishii tu katika matumizi ya lugha. Mtu mweusi anapofika Ufaransa habadilishwi na lugha tu. Anabadilishwa pia kwa sababu ni kutoka

Ufaransa ambapo amepata maarifa yake kuhusu Montesquieu, Rousseau, na Voltaire, lakini pia kwa sababu Ufaransa inampa tabibu wake, mkuu wake wa idara, watendaji wengine wengi wasiohesabika. Kwa hivyo, suala sio lugha tu, bali pia ustaarabu wa mtu mweupe (Fanon, 2008: xv) (Tafsiri yangu)..



*Kielelezo: Punda anayevutwa na mtoto wa Kizungu*  
Chanzo: Mwandishi kwa msaada wa AkiliUnde

Katika hoja hii, Fanon anaiangalia lugha (ya Kifaransa) kama kanzi yenye kubeba vipengele vingi ndani yake. Inabeba alama ya kusoma au elimu kwa ujumla, fahari ya fasihi na sanaa, ujuzi wa utabibu, madaraka na ukuu katika nafasi za kiutendaji kwani mwenye kujua anainuliwa kutoka katika ujinga na kupewa elimu. Vipengele vyote hivi huwa ni sifa ya lugha yoyote ile duniani. Lakini, watawala wa kikoloni waliwaaminisha watawaliwa kudhani kuwa sifa hizi za lugha zimo katika lugha za kikoloni tu. Kuamini huku kunakoendelea kupitishwa katika sera, kanuni na sheria mbalimbali dhidi ya lugha za asili, kunamwacha Mwafrika kubaki kama punda ambaye hawezi kupiga hatua bila ya kuvutwa au kuongozwa na kamba iliyo shingoni mwake. Leo katika Afrika huru, mtu mweusi, mtumwa, anafananishwa na punda mkubwa aliyefungwa kijikamba kidogo sana huku akivutwa na kitoto cha Kizungu. Hajui anapelekwa wapi lakini ana imani kuwa bwana wake huyo anampeleka mahali pazuri penye nyasi nyororo ale.

Ingawa punda huyu amefungwa kamba, lakini kwa hakika kamba iliyo na nguvu zaidi ni iliyo mawazoni. Hali hii ndiyo inayotokeza minyiri ya utumwainashika zaidi fikra kuliko mwili halisi. Utumwa wa kifikra ni mbaya zaidi kuliko utumwa wa kimwili. Wakati utumwa wa kimwili hutumia nguvu, shuruti, fimbo, ukatili na maumivu makali kwa watumwa, utumwa wa kifikra huingizwa taratibu kupitia katika sera za lugha, sheria na kanuni zinazohusiana na lugha (Fanon, 1963); na aghalabu mtumwa hujikuta akitii bila shuruti. Misingi ya dhana ya kutii bila shuruti inachochewa zaidi na mhimili wa dini (Marley, 1980). Dini,

kupitia vitabu vya imani, hutokeza lugha inayoelekeza utiifu na kutokuhoji huku ikitanguliza rai kuwa “Mungu” mwenye nguvu na mamlaka huchukia wasiotii, na ndiye Mungu anayejalilia uhai au kuondoa uhai kwa kila kiumbe (wa Thiong’o, 1986; Mbembe, 2001; Wynter, 2003;).

Kuhusiana na lugha, iliaminishwa awali kuwa mawazo ya “Mungu” huyu yaliletwa kupitia lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu au Kireno. Mawazo ya Mungu wa Kiafrika yalionekana si ya kistaarabu. Aidha, kama ilivyosemwa, ni mawazo ya kishenzi (Vilhanová, 2007; Manala, 2013) ambayo hayakuwa na budi kuachwa au kuzuiwa kwa njia nyingi ili yasienee. Lugha hii ya imani, iliyopitishwa na inayoendelea kupitishwa katika fumbo la imani ilifubaza mawazo ya watumwa na kuwafanya wafikirie kuwa walikuwapo ili wawe watumwa. Ni lugha iliyoendelea kuwalaghai watawaliwa wakati wa ukoloni mkongwe ili milango ya unyonyaji iendelee kuwa wazi kwa faida ya wanyonyaji. Sehemu ifuatayo inajadili kwa kifupi kipengele cha lugha katika ujumla wake na jinsi kilivyopalilia kuwapo kwa utumwa-lugha.

### **3.0 Lugha kwa Ujumla na Ilivyotumika wakati wa Biashara ya Watumwa**

Suala la lugha kwa ujumla limeangaliwa kwa namna mbalimbali kuanzia mawazo ya dhana yenyewe, lugha, hadi mawazo ya lugha mahususi. Kwa kuihusisha lugha na utumwa, Pargas na Schiel (2023: 7) wakiongelea uhuru uliokosekana katika dhana ya utumwa, wanaeleza:

Lugha ya dhana ya uhuru kwa kweli haikuwapo katika miktadha mingi ya utumwa, na hata pale ilipokuwepo, haikuwa mara zote ikimaanisha kinyume cha utumwa (Tafsiri yangu).

Hapa ingawa anaongelea dhana ya uhuru miongoni mwa watumwa, lakini anaonesha kuwa lugha waliyoiongea na kuchunguza ilikuwa na viashiria vinavyoweza kuonesha uhuru au kuonesha utumwa. Kwa maneno mengine, uchunguzi wake unaonesha kwamba maneno yanayoweza kuonesha uhuru hayakuwamo katika msamiati wa watumwa (au labda hayakuruhusiwa kuwapo, au yalififizwa ili yasionekane). Baada ya kushikwa kikatili na kupelekwa utumwani katika hali ya tabu na dhiki, watumwa waliaminishwa kuwa hali hiyo ni jaala. Mungu “aliwaumba” wawe hivyo na anawataka kuendelea kuwamo katika hali hiyo. Walizoezwa kuwa na lugha inayoondoa msamiati wowote kuhusu uhuru. Katika utafiti mwingine, Karev anaihusisha lugha na utumwa kwa kusema:

Kuufikiria muktadha wa utumwa ndani ya mambo ya kijamii na kisheria ya Wamisri unatuhitaji tutambue unyonyaji uliomo katika utumwa na ile biashara ya kumfanya binadamu kuwa bidhaa na vilevile uhalali unaofanywa na Wamisri kupitia lugha ya uzalendo na kulinda biashara hiyo (Karev, 2023: 57) (Tafsiri yangu).

Kwa kusema hivyo, Karev anaona kuwa lugha ilitumika kuendeleza utumwa kwa kisingizio cha uzalendo na uchumi. Biashara ya watumwa ilikuwa ikiwaletea fedha

nyingi wale waliokuwa na watumwa. Biashara hii ilishamiri kiasi cha kuufanya utumwa kuwa wenye kurithiwa, kwa kuwa pia wenye watumwa walikuwa na hadhi katika jamii wakifurahia kuwamo katika tabaka la juu. Lenski anaeleza kwamba:

Kuzaliwa utumwani kwa ujumla kulifanya mtu awe mnyenyekevu na mwenye kudhibitiwa kuliko wageni au mateka kwa sababu watumwa wa asili walilelewa katika mila na lugha za mahali hapo na hawakuwahi kujua maisha yoyote nje ya utumwa (Lenski, 2023: 89) (Tafsiri ni yangu)

Watumwa hawakuruhusiwa kuwa na lugha yao, msamiati wa uhuru na kuongea au kutumia lugha yao kwa namna yoyote ile. Arends (2017) anaeleza kuwa kutokana na kuzuiwa kuwasiliana kwa lugha zao, watumwa walianzisha msimbo wa siri ambapo walikuwa ama wakiwasiliana kwa kupiga mbinja (miluzi) au kwa kuimba. Leo ingawa hakuna utumwa-mkongwe, bado sheria, sera na kanuni za “*Speak English only*”, “*No English, No service*” (Bunyi, 1999; Brock-Utne, 2007, 2010; Pinxteren, 2022) ni mwanngwi wa utumwa huo mkongwe uliozizuia lugha za asili za watumwa. Vizuizi vya lugha za asili kwa waliotawaliwa na Waingereza ni sawa na vile vilivyomo katika jamii zilizotawaliwa na Wafaransa au Wareno. Sheria, sera na kanuni zinazowekwa dhidi ya jamii zenye lugha zao za asili ni vizuizi vilevile kama vilivyokuwapo wakati wa utumwa mkongwe.

Akilinganisha vipengele vya isimu ya lugha kati ya Kilatini na lugha za wenyeji wa Mediterani, Schiel anaonesha kuwa kulikuwa na tofauti za lugha inayohusiana na watumwa baina ya Waislamu na Wakristo. Kwa mfano, anaonesha kuwa nomino dhahania ya *schiavitù* au *esclavitud* katika lugha za kienyeji za Ukanda wa Mediterania ya Magharibi ilijichomoza katika utumwa wa Waislamu na haikutumiwa kamwe kama lugha ya shughuli za kitumwa miongoni mwa kaya za Kilatini (Wakristo). Hata hivyo, watumwa walioishi katika kaya za Kilatini, kwa asili waliitwa (kutegemea jinsia): *schiavo/schia* au *esclavo/esclava*. Mwanamume wa Kiislamu alichukuliwa kuwa ana watumwa, wakati mwanamume Mkristo alichukuliwa kama baba wa familia aliyewatunza watu wote wa nyumbani kwake wakiwamo na watumwa (Pargas na Schiel, 2023).

Hapa lugha inaonesha matabaka ya jinsi dini zilivyoangaliwa zikihusishwa na utumwa. Kwa Waislamu, ilionekana dhahiri ni wenye watumwa. Kwa Wakristo, hata pale walipokuwa na watumwa majumbani mwao kama ilivyokuwa kwa Waislamu, wao walionekana na kuitwa “Baba wenye nyumba” au “Baba watunza familia”. Tofauti hizi baina ya maneno zinaonesha wazi kuwa lugha iliyoambatana na mifumo ya kijami na dini ilitengeneza matabaka yaliyoonesha au kusisitiza utumwa. Ubaguzi huu ulioegemea katika dini, unaonesha kuwa suala la lugha kuhusiana na utumwa na watumwa lilihusiana na dini ambazo pia ndizo zilizotumika kumlaghai mtumwa kifikra. Akichunguza nyaraka kuhusiana na Ukristo, Antwi (2018) anaonesha kuwa Ukristo wa Uyahudi na Ukristo wa Roma uliathiri uelewa wa kanisa kuhusu utumwa. Anaonesha kuwa kutokana na

kuchukuliwa kuwa ni biashara iliyoliingizia kanisa mapato, utumwa ulihalalishwa na kanisa kinyume na msingi wake wa upendo kwa binadamu wote (Antwi, 2018).

Kipengele hiki cha dhima ya dini na lugha katika utumwa hakina budi kufanyiwa utafiti wa kina ili kudhihirisha pasi na shaka, tofauti zilizomo katika dhana ya utumwa na shughuli zinazohusiana na utumwa miongoni mwa dini na lugha mbalimbali. Msimamo huu unaungwa mkono na utafiti wa Kalb anayeeleza nafasi ya lugha katika kuufafanua utumwa. Kalb anasema:

Kutegemeana na muktadha, lugha inayotumiwa kuelezea hadhi ya kuwa mtumwa inaweza kuingiliana na lugha inayotumika katika utolewaji huduma, katika udugu au ufuasi; inaweza pia kwa makusudi kuonekana yenye kutokueleweka vizuri. Ingawa hii inatoa njia inayoweza mchunguzi kuanza kufikiria maana ya utumwa (iwe maana ya kisitiari, au maana kama inavyotumika) katika miktadha mbalimbali ya Asia ya Kusini, lakini pia inajumuisha changamoto inayoweza kuwapata watafiti wa kisasa katika kuwatambua watumwa wenyewe hasa ni kina nani (Kalb, 2023: 530) Tafsiri yangu).

Kwa vyovyote vile iwavyo, lugha inahusiana sana na kusababisha utumwa, kuzuia utumwa au ni matokeo ya utumwa. Lugha inaweza kutumika kuhalalisha utumwa au ikatumika kuwazindua watumwa ili wajikomboe kutoka utumwani. Kama anavyosema Radhi (2020), lugha huonesha njia ya kupata maarifa ambayo hutumika kuzindua akili, na mtumwa kuweza kujikomboa. Baada ya kuangalia lugha katika ujumla wake, sasa sehemu inayofuata inajadili jinsi lugha ilivyojitokeza kuhusiana na biashara ya utumwa wakati wa Waarabu na Wareno.

### **3.1 Lugha wakati wa Biashara ya Utumwa ya Wareno na Waarabu**

Inafahamika wazi kuwa wakati wa utumwa wa Wareno na Waarabu, lugha ilitumika kuufanikisha utumwa. Kupitia kwa wakalimani (Fayer, 2003), lugha iliwezesha wafanyabiashara kufanya biashara ya kupata watumwa. Lugha iliubeba utumwa. Aloyisius Cadamosta aliyepieleza na kuandika habari za upwa wa Afrika Magharibi kati ya miaka ya 1455 na 1456 na kunukuliwa na Fayer (2003: 281), anaeleza hivi akionesha lugha ilivyotumika kuwezesha utumwa:

Kwa kila moja ya melikebu zetu kulikuwamo na mtu mweusi mkalimani ambaye aliletwa kutoka Ureno ambaye alikuwa ameuzwa na Manyampala wa utumwa wa Senegali kwa Wareno wa mwanzo “kuivumbua” nchi hii ya watu weusi. Watumwa hawa walifanywa Wakristo huko Ureno na walifahamu kuongea Kihispaniola vizuri (Tafsiri yangu).

Hapa inaonesha kuwa lugha iliwezesha kufanyika kwa utumwa ambapo wazungumzaji watumwa walikuwa wakalimani wakihusisha lugha ya Kihispaniola na lugha za wenyeji wa Senegali. Kwa upande mwingine, inapoelezwa kuwa watu hawa walifanywa Wakristo kabla ya kuitumikia kazi ya kuwaingiza ndugu zao

katika utumwa, tunadokezwa dhima ya dini, kama tulivyoeleza kabla, kuwa dini ya Ukristo ilitumiwa na baadhi ya viongozi wa dini kuzipumbaza fikra na taratibu kuingiza minyiri, na hasa minyiri ya kifikra ambayo haikuwa vyepesi kuikata. Watawala ambao wengi waliibuka kutokana na biashara ya utumwa, waliwatumia wakalimani ama kupata watumwa zaidi au kuelewa mipango ya watumwa. Fayer (2003: 282) anaeleza hivi kuhusiana na ukalimani na utumwa:

Mwaka 1494 Hicronimus Miinzer aliandika kuwa Mfalme wa Ureno aliwashikilia Waafrika wa rangi tofauti ambao waliweza kuongea Kireno ili waweze kuongea na watumwa wapya waliokuwa wamekamatwa (Fayer, 2003:282) (Tafsiri yangu).

Kama ilivyokuwa katika lugha ya Kireno au Kihispaniola, ndivyo ilivyokuwa katika lugha ya Kiarabu. Waarabu walioshiriki katika biashara ya utumwa walilazimisha maneno ya Kiarabu katika azma yao ya kubidhaisha watumwa. Pia, kama ilivyokuwa kwa Wareno au Wahispaniola, dini kwa Waarabu ilitumika kama njia ya kuwalainisha, kuwateka kifikra na kuwapumbaza watumwa. Maneno mengi ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu ni ya kidini, na yale yanayoonesha ubwana na utwana (Fattakhova na Mingazova, 2015). Katika utafiti wao, Chiraghdin na Mnyampala wanasema kuwa kuwamo kwa maneno mengi ya mkopo katika Kiswahili kutoka katika Kiarabu kunaonesha jinsi Kiarabu kilivyotumika kufundisha dini ya Kiislamu (Chiraghdin na Mnyampala, 1977).

Kwa hiyo, lugha za wale waliohusika katika biashara ya utumwa zilitumika sana kuufanikisha utumwa. Vilevile, lugha hizo zilitumika baadaye katika kuuendeleza utumwa. Akiongelea watumwa waliotoka sehemu za Afrika Mashariki kupelekwa Uarabuni, Hopper (2015: 18) anasema:

Watumwa wapya iliwabidi kujifunza lugha ya bwana wao ili wapate hadhi mpya na waweze kuelewana na matakwa ya mabwana zao wenye watumwa ili hatimaye waweze kuthaminiwa kama watumwa (Tafsiri yangu).

Nukuu hapo juu inaonesha dhima changamani ya lugha ambayo si tu kuwasiliana na kuelewana, bali hata kurubuniwa. Kupata hadhi ni aina ya kurubuni kwa upande mmoja na kudunisha kwa upande wa pili. Mtumwa anarubuniwa kuwa akipata lugha fulani, atakuwa na hadhi. Kwa upande mwingine, mtumwa anadunishwa kwani hata kabla hajawa mtumwa alikuwa na hadhi yake kama binadamu kamili. Lakini, anawekwa katika mazingira yanayoonesha kuwa hana hadhi yoyote, na ili “apewe” hadhi ni lazima akubaliane na matakwa ya bwana mwenye watumwa. Matumizi ya lugha katika kutengeneza utumwa, hasa wa kifikra, yaliendelea hata baada ya utumwa wa kimwili. Wakati wa ukoloni mkongwe, lugha za kikoloni zilijenga matabaka ya kitumwa. Hata sasa, taratibu tunaanza kupata dhana mpya ya utumwa ambao unakuwa ni zaidi ya ule wa kimwili.

Minyiri ya utumwa-lugha inajiviringa na kuwavunganiza watumwa kifikra na kuwafanya kwanza wasitambue kuwa walikuwa na hadhi kabla hawajashikwa na

kuingizwa utumwani na pili utumwa-lugha unawafanya wajikane. Hatua hii ya kujikana, wakati wa ukoloni mamboleo, inasababisha utumwa-lugha kuathiri fikra ya aliyetawaliwa. Mtawaliwa anashikwa na minyiri ya kikoloni kiasi cha kujikuta katika mtanziko: alikotoka hakujui, na kama kuna aendako, hakufahamu. Biashara ya utumwa ya Wareno na Waarabu barani Afrika (Gakunzi, 2018; Caldeira, 2024) iliyotokea kwa karne nyingi, ilihusisha kutekwa na kusafirisha kwa watumwa nje ya Afrika. Tunaweza kuangalia dhima za lugha katika kufanya utumwa, kuuendeleza na kuukuza kibiashara na kijamii katika vipengele vifuatavyo:

Katika nyakati mbalimbali tofauti, na kwa kutumia mbinu tofauti, wafanyabiashara wa Kireno na Kiarabu waliwasiliana na mawakala wa utumwa pale walipotaka kufanya biashara ya watumwa. Kwa hiyo, hapa dhima ya lugha ni ile ya mawasiliano. Ikumbukwe kuwa, watumwa wengine walioingizwa utumwani walikuwa wakishikwa kwa nguvu, kwa kuvamiwa na kutekwa.

Wale walionunuliwa, kulikuwapo na mawasiliano ambayo yanaonesha lugha ya ulaghai ilivyotumika na hata pengine ahadi za kupata utajiri (Caldeira, 2024). Kiarabu, kama lugha ya mawasiliano pwani na kisha ndani ya bara, mara nyingi kilitumiwa kati ya makabila tofauti kwa kuchanganya lugha za asili na maneno ya Kiarabu. Mawasiliano haya yaliruhusu mitandao ya biashara kuenea katika maeneo mbalimbali ya Afrika. Kutokana na kipengele hiki cha mawasiliano, kulitokeza kijitabaka kingine ambacho nacho kiliinuka kibiashara kutokana na lugha. Kijitabaka hiki kiliibuka kwa kuichukulia lugha kama bidhaa iliyowalipa, hivyo, wakatokea wachuuzi-lugha.

Mara nyingi, wafanyabiashara ya utumwa iliyofanywa na Waarabu walitegemea mawakala wa ndani ya Afrika ambao waliweza kuzungumza Kiarabu na lugha za Kiafrika. Mawakala hawa walitumia ujuzi wao wa lugha kufanya biashara na ndio tunaawarejelea hapa kama tabaka la *wachuuzi-lugha*. Wao hawakuhitaji watumwa.



Kielelezo Na. 2: *Sanamu za watumwa huko Zanzibar*

**Chanzo:** Picha na mwandishi, Zanzibar

Mwakala walihitaji fedha ya Mwarabu. Waliitumia lugha kufanya uchuuzi. Wachuuzi-lugha hawa walikuwa na dhima katika kuwezesha shughuli za watumwa na kuhakikisha kuna mawasiliano mazuri kati ya wafanyabiashara wa Kiarabu na wauzaji wa Kiafrika. Tabaka hili lilikua kibiashara na kuonekana miongoni mwa wanajamii. Lilikuwa tabaka lililokuwa kati ya Waarabu na Waafrika waliowashika wenzao ama kwa kuwalaghai au kwa lazima na kuwatia utumwani.

Mbali na dhima hii ya lugha, kulijitokeza pia kipengele kingine tunachokichambua kama sehemu ya mchango wa lugha katika utumwa. Kipengele hiki ni cha uandishi. Hapa dhima ya lugha inaangaliwa kutokea katika maandishi. Wafanyabiashara wa Kiarabu walikuwa wakiandika na kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi” yaliyohusiana na biashara ya utumwa. Kumbukumbu hizi zilihifadhiwa katika hati za Kiarabu. Waliweka kumbukumbu kuhusu ununuaji, mazingira ya kununua, fedha zilizotumika na miamala yote kwa ujumla ikijumuisha kununua na kuuza watumwa (Ralph, 1992, 1988, 1979). Rekodi zilizoandikwa ziliwasaidia wafanyabiashara wa Kiarabu kufuatilia shehena zao za binadamu na miamala ya kifedha, kutoka Afrika hadi kule walikopelekwa (Mario, 1982). Hapa tunaona dhima nyingine ya lugha katika utumwa, kutoka katika lugha ya mazungumzo hadi lugha ya maandishi – lugha inatumika kutunza kumbukumbu za biashara ya watumwa. Mbali na lugha ya maandishi katika kuwezesha biashara ya utumwa, kipengele kingine kilichojitokeza hasa kwa Waarabu kilikuwa lugha inayoonwa kupitia katika dini.

Kama ilivyosemwa kabla, katika baadhi ya maeneo wafanyabiashara wa Kiarabu waliwateka watumwa wao kifikra na kuwasilimisha (Alexander 2001;

Fadel, 2024). Mtumwa aliaminishwa kuwa kule aendako anakwenda kuwa mtu mpya, mwenye fikra na imani mpya ya Kiislamu itakayomfanya awe na hadhi zaidi (Vernet, 2009). Kwa hiyo, watumwa walirubuniwa kusilimu. Fikra za mateka hao wa Kiafrika zilibadilishwa taratibu kutoka katika kukataa na kugoma kutekwa hadi kukubali na pengine kujipeleka wenyewe ili kusilimishwa. Waliacha imani zao za jadi za Kiafrika na kushika njia mpya ya imani, wakawa Waislamu (Fadel, 2024). Uhusiano uliopo hapa ni kuwa, mabwana wa Kiarabu waliitumia lugha ya Kiarabu kuwafundisha watumwa imani ya Uislamu. Kujifunza Kiarabu mara nyingi ilikuwa sehemu ya mchakato huu wa uongofu, kwani uliwawezesha Waafrika waliokuwa watumwa kushiriki katika desturi za kidini za Kiislamu na kuwasiliana vyema na watekaji wao. Kupitia katika lugha ya Kiarabu waliaminishwa kuwa Waarabu watekaji ni watu wazuri ambao wanawatakiwa maisha mema huko waendako ambako hakukujulikana. Mateka watumwa walifundishwa lugha mpya ya Kiarabu na kuingizwa katika dini mpya ya Kiislamu, hata haikuwa rahisi kutofautisha lugha ya Kiarabu na dini ya Uislamu. Vipengele hivi viwili, lugha na dini vilitokeza “faida” nyingine kwa Waarabu wanaofanya biashara ya utumwa.

Kwa kufundishwa lugha ya Kiarabu, iwe ni kwa ulaghai au ushawishi, watumwa walitengwa na wenzao. Kwa kusilimu na kuwa na dini mpya, watumwa walikuwa wanatengwa mbali na dini zao. Vipengele hivi viwili, lugha na dini, vilitumika katika kuwatenga watumwa ili wadhibitiwe vizuri zaidi. Kwa kulazimisha lugha ya Kiarabu kwa Waafrika waliokuwa watumwa, Waarabu wamiliki wa watumwa waliweza kudumisha kiwango cha udhibiti na kuwatenga watumwa wasiweze kuwasiliana. Mahali pengine ikawa ni marufuku kuongea lugha ambayo mmiliki wa watumwa haifahamu (Frazer, 2000; Arends, 2017). Adhabu ya jambo hilo ingeweza kuwa ni kifo (Bouzan, 2021). Vizuiji vya lugha vinaweza kuifanya iwe changamoto zaidi kwa watu walio katika utumwa kuwasiliana na kupanga upinzani. Kwa kuwaingiza katika imani za Uislamu, watumwa walitengwa na wenzao kiimani na hata kiitikadi. Kwa hakika, ndugu zao hawakuonwa kuwa ni ndugu bali ni makafiri, waliopotea na ambao walihitaji wote kusilimishwa na kuwa katika dini mpya ya Uislamu. Vipengele hivi vyote vikiangaliwa kwa pamoja vinaibua kipengele cha dhima ya lugha katika kuujenga na kuuimarisha utamaduni.

Watumwa walifundishwa lugha ya Kiarabu na kupitia katika lugha wakajifunza mambo mbalimbali kuhusu utamaduni wa Kiarabu, ukiachilia mbali suala la dini. Katika ujumla huu, kulikuwa na kukua katika uhusiano wa kitamaduni kwa Waafrika waliofanywa watumwa na kupata hadhi ya kipekee ndani ya jamii ya Waarabu. Lugha iliwapa hadhi watumwa wakaonekana ni wenye hadhi ya kipekee kuliko watumwa ambao hawakuwa Waislamu. Lakini, kwa kuwa utumwa ulionekana kuwa biashara iliyoleta fedha na wenye watumwa wakionekana kuwa ni wenye fedha, kulijitokeza kipengele kingine kilichohusishwa na sheria. Wafanyabiashara ya utumwa wa Kiarabu, wakati mwingine, walitumia maandiko ya Kiislamu ya kisheria na kidini yaliyoandikwa kwa Kiarabu ili kuhalalisha utumwa, wakidai kuwa umeidhinishwa na Uislamu (Esseissah, 2016; Brown, 2019).

Maandishi haya yanaweza kutumika kama aina ya uhalalishaji wa kiitikadi kwa biashara.

Pamoja na hoja hizi kuhusiana na lugha na utumwa, ni muhimu kutambua kwamba biashara ya Waarabu ya utumwa ilikuwa jambo changamani na lenye sura nyingi. Lugha ilichangia katika kuwezesha karibu katika kila kipengele cha biashara hiyo. Tuliyojadili kuhusiana na utumwa wa Waarabu, tunayajadili pia tukiangalia dhima ya lugha wakati wa ukoloni wa Wazungu barani Afrika. Tunajadili jinsi lugha ilivyojenga matabaka ya kijamii, na hasa kiuchumi na kuwatenga watu waliokuwa jamii moja ambayo kwa ujumla ilifanana katika mila na desturi.

#### **4.0 Wakati wa Ukoloni Mkongwe na Nafasi ya Lugha za Kiafrika**

Kwa mujibu wa Ocheni na Nwankwo (2012), kipindi cha ukoloni tunachokijadili ni kile cha kutoka miaka ya 1800 hadi miaka ya kati ya 1960. Ni kipindi ambacho kilibeba ukoloni uliokolezwa na ubeberu. Ni kipindi ambacho lugha za kigeni zilitumiwa kama chombo cha kutenganisha watu na kuimarisha uhibititi wa kikoloni, hata kabla ya kuigawa Afrika kwa kuweka mipaka ya kijiografia na kuanza kuitawala kutokana na matokeo ya mkutano wa Berlin mwaka 1884/1885. Matumizi haya ya lugha za kigeni yalikuwa sehemu ya mkakati mpana wa ubeberu wa kitamaduni uliolenga kuwatawala Waafrika kifikra na hatimaye kiuchumi. Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispaniola zililenga mwisho huo wa kuitawala Afrika kiuchumi (Phillipson, 1992, 2012; Kamalu, 2019). Ubeberu wa lugha ulikuwa na njia maalumu ambazo ulizitumia kuimarisha utumwa wa kifikra (Kamalu, 2019). Kutoka katika utumwa wa kimwili, wakoloni wakawaingiza Waafrika katika utumwa wa kifikra wakati wa ukoloni mkongwe. Njia ya kulazimisha lugha za kigeni ilikuwa kwanza ni kuvunjavunja utamaduni, mila, maarifa na falsafa za Kiafrika ili kuingiza tamaduni ngeni zilizobebwa na lugha ngeni. Wizara ya Habari ya Misri (1985: 18) inaandika hivi kuhusiana na hili:

Msingi wa madai ya Wazungu wakati wa Mkutano wa Berlin na kipindi cha ubeberu kilichofuata ulikuwa ni kutengeneza sera itakayozilazimisha jamii za Kiafrika kuanza kuishi kulingana na matakwa ya watawala wa kizungu. Kuishi ambako hakungetokeza upinzani dhidi ya utawala huo (Tafsiri yangu).

Kwa hiyo, tunapojadili suala la lugha ni muhimu liangaliwe kama sehemu ya mkakati mpana wa kuu utamaduni na utambulisho wa Afrika na kujenga utambulisho na utamaduni wa nchi zilizoitawala Afrika. Zipo njia kadhaa zilizotumika kuhakikisha mkakati huo unafanikiwa. Vipengele vifuatavyo vinaangalia njia hizo ambazo nyingi kati ya hizo zipo hata leo zikiendeleza mkakati uliobuniwa katika mkutano wa Berlin.

Njia ya kurasimisha lugha moja (ya kibeberu) na kuzibeza nyingine (za asili) au kuzipiga marufuku lugha za asili, ilikuwa mkakati wa kwanza wa kuutibua utamaduni wa Kiafrika na baadaye kuuua kabisa. Mkakati huo usingeweza

kukamilika siku moja, na kwa hakika, bado umo katika kukamilishwa hadi leo. Nchini Tanzania, kwa mfano, bado ziko shule ambako watoto hupewa adhabu kama kuvalishwa vigunia shingoni au kuvaa vibao vinavyowatambulisha na kuwabeza kuwa ni wajinga kwa kuwa wameongea Kiswahili (Lyimo, 2015; Qorro na John, 2023). Katika shule hizo, kisingizio ni kuwa uongozi wa elimu shuleni unawahimiza wanafunzi kuongea Kiingereza tu wawapo shuleni, kwa kudhani kuwa kufanya hivyo ni kukuza lugha ya Kiingereza (Akaka, 2013; Mushumbwa, 2022). Hii inaonesha kwa kiasi kidogo tu, ni kwa namna gani minyiri ya utumwa-lugha ilivyowafunga wanaotoa uamuzi kama huo dhidi ya lugha zao wenyewe. Wakoloni wa Ulaya walilazimisha lugha zao ziwe rasmi katika utawala na elimu. Kwa mfano, Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispaniola zilifanywa kuwa lugha kuu zilizomwakilisha Mwafrika katika maeneo ya utawala na katika utoaji wa elimu (Hameso, 1997; Babaci, 2016). Njia hii ilikuwa na matokeo kadhaa:

Mosi, matokeo yanaonekana kupitia katika elimu ya kibaguzi. Wale ambao wangeweza kupata elimu katika lugha rasmi za kikoloni walikuwa pia na faida ya kupata ujuzi na maarifa ambayo yaliwawezesha kuwa na fursa bora za kijamii na kiuchumi. Kutokana na elimu hii iliyofungashwa katika lugha za kikoloni, kukatokea matabaka. Kukawa na tabaka la "wasomi wa kikoloni," waliopata kazi ofisini na kuwa watawala. Hawa walikuwa wachache ikilinganishwa na tabaka la pili ambalo ni idadi kubwa ya watu ambao hawakuweza kupata elimu kama hiyo. Wasomi hawa wa elimu ya Magharibi, wakati mwingine, ndio waliotumiwa na wakoloni kuendeleza sera za kikoloni katika Afrika huru. Walikuwa wameandaliwa kukumbatia na kukuza utamaduni na maadili ya kikoloni, na waliendeleza fikra hizo pengine bila kujua kuwa walikuwa wanaua mashina yaliyowashikilia na kuujenga utu wao. Baadhi ya hawa ndio ambao hutumiwa na wakoloni wa zamani kuvuruga amani na uchumi wa nchi zinazojitahidi kuujenga uchumi wa nchi zao huru.

Umahiri katika lugha za kikoloni ukawa alama ya hadhi na upendeleo wa kijamii. Wale walioweza kuzungumza lugha ya kikoloni kwa ufasaha mara nyingi walionekana kuwa "wastaarabu" zaidi (Kampf, 2019) na walipata nafasi za kazi mbalimbali kwa upendeleo. Kutokana na sera za lugha zilizochipukia wakati wa ukoloni, wale waliokuwa wanazijua lugha hizo si tu walionekana wastaarabu, bali walionekana wana akili kuliko wale ambao hawakuweza kuongea lugha hizo. Ujuzi wa lugha za kikoloni ukawa alama ya hadhi na kupata upendeleo toka katika kijamii.

Pili, mbali na upendeleo huu, walioongea lugha za kikoloni ndio waliopata ajira rasmi na kuitwa "wasomi". Katika makoloni, ujuzi wa lugha za kikoloni ulikuwa sharti mojawapo la kuajiriwa na serikali za wakoloni (Shizha, 2011; Matasci, 2020) na kushiriki katika kuendeleza utawala wa kikoloni. Hii ilimaanisha kwamba watu ambao walikuwa na ujuzi wa lugha hizi walikuwa na uwezekano mkubwa wa kushikilia nyadhifa za mamlaka na ushawishi.

Mbali na lugha, njia ya pili ilijikita katika taratibu za kikoloni zilizoegemea katika kukuza ukabila au kukuza rangi ya kundi fulani la kijamii. Mamlaka ya kikoloni wakati mwingine yaliuina ukabila na kuwagawa wenyeji na pengine

kuunda uhasama baina yao kwa vigezo ama vya lugha au utamaduni tofauti, ilimradi kwa kufanya hivyo wao (wakoloni) wafaidike na utengano utakaotokea baina ya wenyeji walioathirika (Tikumah, 2023). Wenyeji wa nchi ya Rwanda walitengwa baina ya Watusti na Wahutu na wakoloni kuchochea mtengano huo kwa faida za watawala. Katika kuwatenga hivyo, ilikuwa ni rahisi kwa wakoloni kuwagawanya na kuwatawala (Shyaka, 2025). Tatizo hili la ukabila, lenye mizizi yake wakati wa mkutano wa Berlin, linaangaliwa kuwa ni “kansa” inayoiumiza Afrika hadi leo. Kuhusiana na hili, Wizara ya Habari ya Misri (1985: 19) inaandika hivi:

Wakiongozwa na ufahamu wao kwamba Waafrika wangeungana kurejesha uhuru wao, wakoloni walitumia mbinu yao "Gawanya na Utawale" ili kuhakikisha kuendelea kwa ubabe wao wa kiutawala. Kwa njia hiyo, waliweza kupandikiza kile kinachoweza kuitwa “saratani ya kisiasa”. Kwa bahati mbaya, saratani hii bado inauumiza mwili wa Afrika na inajitokeza kupitia uhasama wa kijamii, au kama walivyopandikiza wakoloni wakiuita uhasama wa "kikabila". Mamlaka na serikali za kikoloni barani Afrika ziliendeleza na kukuza ugonjwa huu (Tafsiri yangu).

Mgawanyiko baina ya jamii kwa kigezo cha lugha na hata uhasama na ugomvi uliojitokeza, na ambao hata baada ya uhuru kuna mahali unajitokeza, ni sehemu ya mkakati mpana wa kusambaratisha umoja wa kiutamaduni wa Afrika (Igboin, 2011; Dimkpa, 2015). Hatua hizi za kupiga marufuku lugha za asili, zilisababisha kumomonyoka kwa urithi wa lugha na utamaduni. Ingawa suala hili lilianza wakati wa ukoloni mkongwe, linaonekana zaidi wakati wa ukoloni mamboleo. Kuhusiana na suala la lugha wakati wa ukoloni mamboleo, Qorro na John (2023: 145) wanaonesha faida ambazo zingepatikana kama lugha za asili au za mataifa zingeruhusiwa: Wanafunzi watajifunza kuheshimu na kuthamini utu wao, na utu wa wengine katika jamii bila kujali kama wamesoma au la. Pia, wataheshimu utamaduni, lugha na utaifa wao kwa kuwaondolea adhabu wanayopewa kwa kuzungumza lugha ya taifa lao au lugha zao za asili. Mawazo ya uzalendo kwa jamii zao na nchi yao yataimarika na mengine kuibuliwa.

Hoja ya Qorro na John (2023), inaonesha kuwa kwa kuzuiwa kuongea na kujifunza kwa lugha za asili, wanafunzi walinyimwa nafasi ya kutambua utu wao na wa wenzao, utamaduni wao na maarifa ambayo hubebwa na lugha zao za asili. Kwa athari hizi, fikra za wanafunzi zilikuwa zikiingizwa katika utumwa, fikra zinazoingizwa kwa kanuni na sheria kuhusu lugha ya elimu. Utamaduni ambao ulibeba ndani mwake maarifa, ujuzi wa kale, thamani na utambulisho wa Mwafrika ulipotea. Kwa hiyo, baada ya lugha za asili kusakamwa, mkakati uliokuwapo ni namna ya kuusambaratisha utamaduni wa Kiafrika, jambo ambalo ni vema tuliangalie kwa undani.

Mara nyingi mamlaka za kikoloni zilikandamiza lugha na tamaduni za kiasili, zikionwa kuwa duni au vikwazo kwa dhamira yao ya kuwastaarabisha Waafrika. Maana halisi ya “kuwastaarabisha Waafrika” ilikuwa kuwakandamiza

wasiweze kuibuka na kujitambua. Ukandamizaji ulifanyika kwa mbinu mbalimbali kuanzia katika kuzuia dini za jadi, kuzibeba na mahali pengine kuzipiga marufuku kwa kutoa adhabu kali dhidi ya kilichoonekana ni “ushenzi”. Kwa hiyo, mbali na suala la lugha za asili kuzuiwa, suala la dini kama ilivyokuwa wakati wa utumwa wa kimwili, linaibuka tena wakati wa ukoloni kupitia shughuli za kimisionari, (Dimkpa, 2015) na matokeo yake yanaonekana hadi leo.

Shughuli za kimisionari zilitumia sana lugha, na hasa lugha za wenyeji – kama sehemu muhimu ya kuandaa majilio ya ukoloni kwa kuwafanya watu kuwa Wakristo. Baadhi ya Waafrika waliuchukulia Ukristo kama fursa ya kupanda juu katika hadhi na kuonekana “wastaarabu” kuliko kuuchukulia kama suala la imani (Ocheni, 2012). Wakristo hawa walibadili namna yao ya kuongea lugha zao na kuiga uongeeji wa wamisionari Wazungu (Vilhanová, 2007; ter Haar, 2009). Hii huenda ndiyo mojawapo ya sababu kuwa baadhi ya waliokuwa Wakristo waligeukia pia dini za jadi au waganga wa jadi ili kutafuta ufumbuzi wa yale waliyokabiliana nayo badala ya kuelekea madhabahuni humo makanisani (Masondo, 2015; Merwe, 2016). Hali hii imeendelea hadi wakati wa kipindi tulichomo cha ukoloni mamboleo.

### **5.0 Suala la Lugha katika Kipindi cha Ukoloni Mamboleo**

Ukoloni mamboleo unajulikana kama kuendelea kwa ushawishi wa kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni kutoka kwa wakoloni kwenda kwa nchi walizozitawala hata pale zinapodai kuwa zina uhuru. Ushawishi huu unakamilishwa kupitia lugha za kikoloni kama msingi mkuu. Vilevile, unapitia katika utegemezi wa kiuchumi na ghiliba za kisiasa. Huu ni upande mmoja, lakini kwa upande wa pili, nchi zilizopata uhuru zingependa kuwa na utambulisho wake na kuenzi utamaduni wake. Katikati ya hali hii, Waafrika wanajikuta wamenaswa kati ya nguvu zinazokinzana, yaani nguvu ya nje ambayo Waafrika wangependa kuipinga na nguvu ya ndani ambayo Waafrika wanapenda kujitambulisha kwayo. Wakati huu wa ukoloni mamboleo kutatizika huku kunafanywa kugumu zaidi kutokana na nguvu ya ushawishi wa lugha za kikoloni. Waafrika wanaokumbatia lugha za kigeni wamebaki kwenye mtanziko, hawajui wanachotaka kama Waafrika na wala hawajui wasichokitaka. Leo hali hii ya ukoloni mamboleo, inaangaliwa kupitia dhana ya utandawazi ambapo inaelezwa:

Kutegemea misaada ya kigeni na kujiingiza kwa mashirika ya kimataifa katika shughuli za kiuchumi na za kijamii barani Afrika kunaonesha kuwa Afrika mwanzoni mwa karne ya 21 bado iko katika hatua ya ukoloni mamboleo. Shughuli hizi za mashirika barani Afrika, hasa mashirika kutoka Ulaya na Amerika zinaonesha wazi kuwa kuna unyonyaji wa kiuchumi na utawala wa kitamaduni (*Afisi, “Ukoloni mamboleo” ht*) (Tafsiri yangu).

Njia kuu ya kufanikisha unyonyaji huu imekuwa ikipitia katika lugha za kikoloni. Lugha hizi zimetumika kuteka fikra za Waafrika wengi na kuingiza mawazo ya kutokujiamini na kutokuthamini lugha za kiasili.

Mbali na kuteka fikra na kuwafanya Waafrika watumwa, lugha za kikoloni zimeendelea kutumika kama chombo cha udhibiti. Lugha za kikoloni kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno zinaendelea kutawala mawasiliano rasmi, elimu, na utawala katika nchi nyingi za Afrika. Utawala huu wa lugha unazipa mamlaka za zamani za kikoloni faida kubwa katika suala la kuathiri maamuzi ya kisiasa na kiuchumi. Kwa Mfano, katika nchi ambazo Kiingereza ndiyo lugha rasmi, kama vile Nigeria au Ghana, viongozi wa kisiasa, wasomi na wafanyabiashara mara nyingi huwasiliana kwa Kiingereza (Ukonu, 2025). Mawasiliano kama haya yanawatenga wale ambao hawajui lugha hizo, na hivyo, wanashindwa kushiriki kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi (Dartey, 2025). Hili huzua mgawanyiko wa kiisimu unaoweza kutumiwa na walio madarakani kwa manufaa ya watawala wa zamani wanaomiliki lugha husika (Hilt, 2017). Katika ukoloni mamboleo, dhana ya utumwa-lugha inajidhihirisha wazi na athari zake zinajitokeza miongoni mwa Waafrika. Ili kufahamu vema suala hili, tuangalie jinsi ambavyo lugha za kikoloni zinajenga utumwa na kutishia mustakabali wa Waafrika, kwa kupitia mawazo ya utumwa-lugha.

### **5.6 Misingi ya Utumwa-Lugha Inavyojitokeza katika Kipindi cha Ukoloni Mamboleo**

Nadhariatete ya utumwa-lugha inaonesha kuwa kulazimishwa kwa lugha za kikoloni katika jamii za Kiafrika wakati wa ukoloni, kulikuwa na athari za kudumu katika utambulisho wa kiakili na kitamaduni wa Waafrika. Nadhariatete hii inaonesha kwamba kulazimishwa kwa lugha za kikoloni kama sehemu ya maisha ya Mwaafrika kumesababisha aina ya utumwa wa kiakili ambapo lugha za asili zinafutwa ama kwa kanuni na sheria au kwa kukosa uchaguzi, mambo yanayosababisha upotevu wa tamaduni, maarifa, falsafa na utambulisho wa asili. Matokeo ya hali hii ni kuishi katika utegemezi na kujihisi duni kila wakati. Ili mchakato huu wa utumwa ueleweke vizuri, tuangalie misingi ifuatayo inayoonesha jinsi utumwa-lugha unavyojengwa wakati wa ukoloni mamboleo.

Kumekuwapo na mmomonyoko wa utamaduni katika jamii nyingi za Kiafrika (Wahab na wenzake, 2012; Obikwelu na wenzake, 2023) katika kipindi cha ukoloni mamboleo. Mwenendo huu unamaanisha kuwa hatua kwa hatua kunatokea kupotea kwa urithi wa kitamaduni. Kupokelewa kwa lugha za kikoloni na kuzifanya kuwa zina hadhi ya juu kuliko lugha za asili, mara nyingi kumamaanisha kuwa Waafrika ni duni. Alama mojawapo ya uduni huu ni kukandamizwa kwa lugha za asili na kufifishwa kwa tamaduni. Hali hii inasababisha mmomonyoko wa maarifa ya kitamaduni, mila simulizi na ujuzi na maarifa ambayo yalipitishwa katika lugha za kiasili kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine, kizazi baada ya kizazi. Utawala wa lugha na tamaduni za kikoloni mara nyingi ulizifanya tamaduni za kiasili kuwa duni, na zisizoweza kuchangia lolote katika maendeleo ya jamii. Hali hii ya kuzidharau lugha na tamaduni za Kiafrika imejenga fikra potofu miongoni mwa Waafrika kuhusu nafasi ya lugha zao, tamaduni zao katika maisha yao na

kuwapo kwao kama Waafrika (Qorro na John, 2023). Uduni huu umeendelea kuwafanya Waafrika kutokujiamini na kuzama katika utumwa wa fikra.

Msingi wa pili unahusishwa na kudhoofika kwa uwezo wa kujieleza. Matumizi na upendeleo wa lugha za kikoloni, hasa kama njia ya kutolea elimu, katika vyombo vya habari, na mawasiliano rasmi ulipunguza uwezo wa Waafrika kujieleza kikamilifu. Kizuizi hiki cha lugha kilidhoofisha kushiriki kwa Waafrika wengi katika mazungumzo yenye kuonesha ujuzi na kuchangia katika siasa na mustakabali wa maendeleo ya kijamii.

Msisitizo mkubwa wa mbinu hii ya kumdhoofisha Mwafrika ni kupitia katika elimu. Wale ambao hawakuwa na ujuzi wa lugha za kikoloni walikabiliwa na hasara ya kutopata elimu na ujuzi uliofungashwa ndani ya lugha za kikoloni. Hali hii kwa wakati wote imezua mgawanyiko kati ya wale ambao wangeweza kupata fursa za ukuaji wa kiakili na kibinafsi na wale ambao hawakuweza. Kundi la ambao wanaonekana hawawezi ni kubwa zaidi na linaloendelea kukua. Kutokana na msingi huu, kunajitokeza changamoto nyingine ambayo tunaorodhesha kama msingi wa tatu.

Msingi wa tatu ni athari zinazotokea kisaikolojia. Kulazimishwa kikanuni na kisheria kwa lugha za kikoloni kuibeba elimu ya Mwafrika kumesababisha tabiahasi ya kujidunisha kwa Mwafrika. Kupendelewa, kulazimishwa na kuzibeba lugha na tamaduni za kikoloni kumeingiza mawazo kwamba lugha na tamaduni za Kiafrika hazina thamani wala nafasi katika kuchangia maendeleo ya Waafrika. Mawazo haya yanachanua kijiitawi kingine kinachozidisha unyonge wa Mwafrika. Kijiitawi hicho ni kuendelea kutegemea mamlaka za zamani za kikoloni, katika nyanja za elimu, uchumi, siasa na tamaduni za kigeni. Vipengele vyote hivi vinakoleza utumwa wa kifikra ambao unapitia katika lugha. Msingi huu, unaiingiza Afrika katika utegemezi mwingine mkubwa na kuendeleza utumwa na unyonge wa Mwafrika. Huu ni utegemezi wa kiuchumi na matokeo yanayoendana na utegemezi huo.

Msingi wa nne unaegemea katika uchumi na ghiliba za kisiasa. Matumizi ya lugha za kikoloni katika michakato ya kisiasa na utawala imekuwa ikiwatenga wale ambao hawana ujuzi wa lugha hizo na hivyo kuwafanya washindwe kushiriki kikamilifu katika maisha ya kisiasa na kiuchumi ya nchi zao (Ukonu, 2025; Dartey, 2025). Matumizi haya ya lugha za kikoloni na matokeo yake yanainyima nchi ya Kiafrika yenye kukumbatia lugha hizo na kuzidharau lugha zake za asili uwakilishi wa utajiri uliomo katika lugha za asili (Munyai na Phooko, 2021). Wananchi wanashindwa kuchangia mawazo katika kuleta fikra za maendeleo kwa vile tu hawawezi au hawataki kutoa mawazo yao kupitia katika lugha za kikoloni. Jambo hili haliishii tu katika kuinyima nchi uasili wake, bali pia kwa wananchi wake kukosa fursa za kuinuka kiuchumi. Upatikanaji wa fursa za kiuchumi mara nyingi umetegemea umahiri wa lugha za kikoloni. Katika nchi nyingi za Kiafrika, ni wananchi wachache wenye kuzijua lugha za kikoloni, na hao ndio huchangia maendeleo ya nchi zao kwa mkabala wa kuutukuza ukoloni na kujibakiza watumwa.

Hali hii ya utumwa wa kifikra unaopitia katika lugha imeendelea kuzisumbua nchi nyingi za Kiafrika baada ya uhuru wa bendera.

### 6.0 Hitimisho

Ni muhimu kutambua kwamba matumizi ya lugha za kikoloni katika utambulisho wa kifikra na kitamaduni wa Waafrika ni suala la utumwa wa kiwango cha kipekee. Kiwango hicho kinagusa masuala ya jamii na hasa uchumi wa nchi zilizofungwa katika minyiri ya utumwa huu. Ingawa matumizi ya lugha za kiasili yanakuzwa katika baadhi ya nchi za Kiafrika kama njia ya kurejesha urithi wa kitamaduni na kukuza fahari ya kitaifa, lakini urithi wa lugha za kikoloni na ushawishi wake umeendelea kuzidumaza nchi za Kiafrika kifikra. Waafrika wengi katika nchi hizi wamo katika mtanziko wa kifikra. Kwa upande mmoja, wangependa kujitambulisha kama Waafrika kwa utamaduni na kwa utambulisho. Lakini, kwa upande mwingine, wamenaswa katika utamaduni wa Kimagharibi unaoambatana na kumbukumbu za ukoloni, na kuwaacha wakizama katika utamaduni ambao si wa popote. Si utamaduni kutoka katika makoloni yao ya zamani na wala si utamaduni wa Kiafrika. Mchakato wa kushughulikia utumwa-lugha unaosukumwa na kuwezesha na lugha za kikoloni ni sehemu ya juhudi pana za kurejesha na kusherehekea utambulisho wa tamaduni za Kiafrika na tofauti zake.

### Marejeleo

- Afisi, O.T. (h.t). "Neocolonialism" *The Internet Encyclopedia of Philosophy*. <https://iep.utm.edu/>
- Akaka, L. (2013). "Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya." *Kioo cha Lugha*. 11: 47-57.
- Alexander, J. (2001). "Islam, Archaeology and Slavery in Africa." *World Archaeology*. 33(1): 44-60.
- Antwi, E.K.E. (2018). "Church Involvement in the Trans-Atlantic Slave Trade: Its Biblical Antecedent vis-à-vis the Society's Attitude to Wealth." *Studia Historiae Ecclesasticae*. 44(2): 1-19. <https://doi.org/10.25159/2412-4265/3245>.
- Arends, J. (2017). *Language and Slavery: A social and Linguistic History of the Suriname Creoles*. Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.
- Babaci, W.Z. na Mchombo, S. (2016). "The Use of African Languages and the Context of Learning in Education." *Current Studies in Comparative Education, Science and Technology*. 3: 12-27.
- Balfour, R. (2002). "Postcolonial Twilight: English as a Failed Lingua Franca." *The English Academy Review*. 19. <https://doi.org/10.1080/10131750285310041>. 20-32.

- Bellagamba, A., Greene, E.S. na Klein, A.M. (Wah.). (2016). *African Voices on Slavery and The Slave Trade*. Juz. 2: Essays on Sources and Methods. Cambridge: Cambridge University Press.
- Bouzan, R. (2021). African Muslim Slaves: Literacy and Arabic Narratives. Master's Theses, Dissertations, Graduate Research and Major Papers Overview. 345. <https://digitalcommons.ric.edu/etd/345>.
- Brock-Utne, B. (2007). "Learning through a Familiar Language Versus Learning through a Foreign Language—A Look into some Secondary School Classrooms in Tanzania." *International Journal of Education Development*. 27: 487-498.
- Brock-Utne, B. (2010). "Research and Policy on the Language of Instruction Issue in Africa." *International Journal of Education Development*. 30: 636-645.
- Brown, J.A.C. (2019). *Slavery and Islam*. London: Oneworld Academic.
- Bunyi, G. (1999). Rethinking the place of African indigenous languages in African education. *International Journal of Educational Development*, 19(4), 337–350. [https://doi.org/10.1016/S0738-0593\(99\)00034-6](https://doi.org/10.1016/S0738-0593(99)00034-6)
- Caldeira, A. (2024). "Portuguese Slave Trade." *Oxford Research Encyclopedia of African History*. <https://oxfordre.com/africanhistory/view/10.1093/acrefore/9780190277734.001.0001/acrefore-9780190277734-e-903>.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi. Oxford University Press.
- Conboy, M. (1990). Attitudes to Languages other than English in the Context of British Nationalism. Tasnifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa)., Chuo Kikuu cha London. <https://discovery.ucl.ac.uk/id/eprint/10018801/1/126197.pdf>
- Dartey, E.A. (2025). "Languages Are Not the Problem: Re-thinking Language Planning in Post-colonial Ghana Through African and Africana Philosophical Frameworks." *Journal of Asian and African Studies*. Juz. 60. Na. 8:1-17. DOI: <https://doi.org/10.1177/00219096251365487>.
- Dimkpa, P. (2015). Colonialism, Independence and Underdevelopment in Africa: The Pre-eminence and Blame Game. Shahada ya Umahiri katika Masomo ya Kiafrika. Chuo Kikuu cha Dalarna, Sweden. <https://www.diva-portal.org/smash/get/diva2:1386410/FULLTEXT01.pdf>. Imesomwa Septemba 2025.
- Egbonu, O. na Isanbor, P.O. (2024). "African Personality: The Place and Role of Language." Katika I.A. Kanu, E.J.O. Ndubisi, N.D. Ulogu, W.M. Eche, F.O. Ejegbavwo (Wah.), Proceedings of 2024 International Conference of *African Heritage, Identity and Sustainability: Navigating Globalization and Post-Colonial Realities*, APAS. Maryland. kur. 80 – 90.
- Esseissah, K. (2016). "Paradise Is Under the Feet of Your Master: The Construction of the Religious Basis of Racial Slavery in the Mauritanian Arab-Berber Community." *Journal of Black Studies*. 47(1): 3-23. <http://www.jstor.org/stable/24572956>.

- Fadel, A. (2024). "Islam, Slavery and Racism: The Use of Strategy in the Pursuit of Human Rights (1987)." *American Journal of Islam and Society*. 41(1): 237-262 •Doi: <https://doi.org/10.35632/ajis.v41i1.3423> .
- Fanon, F. (2008). *Black Skin, White Masks*. Toleo jipya. London: Pluto Press.
- Fanon, F. (1963). *The Wretched of the Earth* (C. Farrington, Trans.). New York: Grove Press.
- Fattakhova, R.A. na Mingazova, G.N. (2015). "Arabic Loanwords in Tatar and Swahili: Morphological Assimilation." *Journal of Sustainable Development*. 8 (1): 302-308.
- Fayer, J.M. (2003). "African Interpreters in the Atlantic Slave Trade." *Anthropological Linguistics*. 45(3): 281-295. <http://www.jstor.org/stable/30028896>.
- Fieser, J., & Dowden, B. (Eds.). (h.t). *Internet Encyclopedia of Philosophy*. <https://iep.utm.edu/>
- Gakunzi, D. (2018). "The Arab-Muslim Slave Trade: Lifting the Taboo." *Jewish Political Studies Review*. 29(3/4): 40-42. <http://www.jstor.org/stable/26500685>.
- Hameso, S. (1997). "The Language of Education in Africa: The Key Issues." *Language, Culture and Curriculum*. 1-13. 10.1080/07908319709525237.
- Hilt, L.T. (2017). "Education without a Shared Language: Dynamics of Inclusion and Exclusion in Norwegian Introductory Classes for Newly Arrived Minority Language Students." *International Journal of Inclusive Education*. 21(6): 585-601. <https://doi.org/10.1080/13603116.2016.1223179>
- Hopper, S.M. (2015). *Slaves of One Master: Globalization and the African Diaspora in Arabia in the Age of Empire*. New Haven: Yale University Press.
- Igboin, O.B. (2011). "Colonialism and African cultural values." *African Journal of History and Culture*. 3(6): 96-103. <http://www.academicjournals.org/ajhc>.
- Kalb, E. (2023). "Slavery in South Africa". Katika, D. A. Pargas na J. Schiel (wahr.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*, 517-534. (eBook) [https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5\\_29](https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5_29)
- Kamalu, N.C. (2019). "British, French, Belgian and Portuguese Models of Colonial Rule and Economic Development in Africa." *Annals of Global History*. 1(1): 37-47.
- Kampf, C. (209). *English in France - Linguistic Dominance and Ambivalence*. Undergraduate Honors Projects No. 745. Chuo Kikuu cha Grand Valley State, Michigan, USA. Imepakuliwa kutoka <https://scholarworks.gvsu.edu/honorsprojects/745>.
- Kanu I.A, Ndubisi E.J.O, Ulogu N.D, Eche W.M, Ejegbavwo F.O. (Wah.). (2024). *Proceedings of 2024 International Conference of African Heritage, Identity and Sustainability: Navigating Globalization and Post-Colonial Realities*, Maryland: APAS.

- Karev, E. (2023). "Ancient Egyptian Slavery". Katika, D. A. Pargas na J. Schiel (wahr.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*, 41-66. (eBook) [https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5\\_3](https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5_3)
- Lenski, N. (2023). "Slavery in the Roman Empire". Katika, D. A. Pargas na J. Schiel (wahr.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*, 87-108. (eBook) [https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5\\_5](https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5_5)
- Lodhi, Y.A. (1993). "The Language Situation in Africa Today." *Nordic Journal of African Studies*. 2(1): 79-86.
- Lydon, G. na Hall, S.B. (2016). "Excavating Arabic Sources for the History of Slavery in Western Africa". Katika A. Bellagamba, E.S. Greene na A.M. Klein (Wah.). *African Voices on Slavery and The Slave Trade*. Toleo la Pili. Essays on Sources and Methods. Cambridge: Cambridge University Press. Kur. 15-49.
- Lyimo, P.L. (2015). "Reading Kiswahili Language at Lower Standards in Public Primary Schools in Kinondoni, Tanzania: Challenges." *Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mabe, E. J. (2020). "The Situation of the Indigenous African Languages as a Challenge for Philosophy." *Philosophy Study*. Juz. 10(10): 667-677. doi: <https://doi.org/10.17265/2159-5313/2020.10.009>.
- Majola, Y.L.P., Mandende, I.P. na Cekiso, M. (2024). "A Linguistic Analysis of Spelling Errors of Selected Indigenous Town and Village Names in the Eastern Cape, South Africa." *Nomina Africana*. 38(1-2): 57–68.
- Manala, J.M. (2013). *The Impact of Christianity on Sub-Saharan Africa*. Paper Presented at the 2013 Africa Conference on Social Movements, Religion, and Political Expression in Africa, Held at the University of Texas at Austin, USA.
- Mario, A. (1982). "Power and Slavery in Central Africa: Chad (1890-1925)," *Journal of Negro History*. 67: 198-211.
- Marley, B. (1980). *Redemption Song*. Katika [Album] *Uprising*. Island Records. (Unarejelewa Kitaaluma kama Matini ya Kitamaduni).
- Masondo, S. (2015). "Indigenous Conceptions of Conversion among African Christians in South Africa." *Journal for the Study of Religion*. 28 (2) 87 – 112.
- Matasci, D., Dores, G.H. na Jerónimo, B, M (Wah.) (2020). *Education and Development in Colonial and Postcolonial Africa: Policies, Paradigms, and Entanglements, 1890s–1980s*. Cham: Palgrave Macmillan.
- Mbembe, A. (2001). *On the Postcolony*. Oakland: University of California Press.
- Mberia, K. (2015). "The Place of Indigenous Languages in African Development." *International Journal of Language and Linguistics*. 2 (5): 52-60.
- Merwe, D. (2016). "From Christianising Africa to Africanising Christianity: Some Hermeneutical Principles." *STJ | Stellenbosch Theological Journal*. 2: 559-587. <https://doi.org/10.17570/stj.2016.v2n2.a25>

- Msakha, M., Harosh, H.E. (2024). "African Language-speaking Plurilingual Students' Writing in English: Shifting the Focus from 'Error' to 'Variation'." *Critical Studies in Teaching and Learning*. CRISTAL, Juz.12 na.2 <https://doi.org/10.14426/cristal.v12i2.2534>
- Munyai, A. na Phooko, M.R. (2021). Is English Becoming a Threat to the Existence of Indigenous Languages in Institutions of Higher Learning in South Africa? *De Jure Law Journal*. 54(1): 298-327. <https://doi.org/10.17159/2225-7160/2021/v54a18>
- Mushumbwa, R.A. (2022). "Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Sekondari za Umma Tanzania: Mfano wa Shule Teule za Sekondari Wilaya ya Kwimba." *Jarida la CHALUFAKITA*. 4: 31-50.
- Nketia, K. J.H (1968). "The Language Problem and African Personality." *Presence Africaine*. Juz. 3 (67) 157 – 171.
- Obikwelu, I.J.; Gérard-Marie, M na Odumegwu, A. C. (2023). "The Effects of Neocolonialism on Africa's Development." *PanAfrican Journal of Governance and Development*, Juz.4 (2), 3-35
- Ocheni, S., Nwankwo, C.B. (2012). "Analysis of Colonialism and Its Impact in Africa." *Cross-Cultural Communication*. Juz. 8, (3): 46-54. DOI:10.3968/j.ccc.1923670020120803.1189.
- Pargas, A.P; na Schiel, J. (Wah). (2023). *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*. Palgrave Macmillan. eBook. <https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5> Springer Nature Switzerland AG.
- Phillipson, R. (1992). *Linguistic Imperialism*. Oxford: Oxford University Press.
- Phillipson, R. na Skutnabb-Kangas, T. (2012). *Linguistic Imperialism and Endangered Languages*. 495-516. <https://doi.org/10.1002/9781118332382.ch20>.
- Qorro, A.S. M na John, P. (2023). "Nafasi ya Lugha katika Elimu Barani Afrika: Suala la Kiswahili na Lugha Zingine za Kijamii Nchini Tanzania," *Mulika*, Na. 42 (2), 139-163.
- Radhi, F.G. (2020). "Language as a Means of Emancipation in Shelley's Frankenstein" *American Journal of Humanities and Social Sciences Research (AJHSSR)* e-ISSN: 2378-703X 4 (9) 43-48.
- Ralph, A. A. (1979). "The Trans-Saharan Slave Trade: A Tentative Census," in *The Uncommon Market: Essays in the Economic History of the Atlantic Slave Trade*, Henry A. Gemery and Jan S. Hogendorn, eds. New York: Academic Press. uk. 23-79.
- Ralph, A. A. (1988). "The 19th Century Islamic Slave Trade from East Africa (Swahili and Red Sea Coasts): A Tentative Census," *Slavery & Abolition*, (9), 21-44.

- Ralph, A. A. (1992). "The Mediterranean Islamic Slave Trade out of Africa: A Tentative Census," *Slavery & Abolition*, (13) 214–248.
- Shizha, E., Kariwo, T. M. (2011). *Education and Development in Zimbabwe: A Social, Political and Economic Analysis*. Brill.
- Shyaka, A. (2025). "The Rwandan Conflict: Origin, Development, Exit Strategies" A Study ordered by The National Unity and Reconciliation Commission. Reseau Documentaire International Sur la Region de Grands Lacs Africains. Online at <http://hdl.handle.net/2152/4746>.
- ter Haar, G. (2009). *Religion and Development. What's in Two Names: Symposium on the 10th Anniversary of the Chair of Religion and Development, 11 June 2009. ISS Staff Group 2: States, Societies and World Development*. Imepakuliwa kutoka <http://hdl.handle.net/1765/40520>
- Tikumah, I, (2023). "The Colonial Creation of Tribalism in Africa(?)" *Social Alternatives*. Juz. 42 No. 1.
- Ukonu, U.E. (2025). English as a Lingua Franca in Nigeria: Its Influence on the Political, Commercial, and Educational Development. Tasnifu ambayo haijachapishwa. No. 1405945639. Chuo Kikuu cha Iceland. Imepakuliwa August 2025 <https://skemman.is/bitstream/1946/48821/1/BA%20THESIS%20.%20UCHECHUKWU%20EME%20UKONU.pdf>
- Van Pinxteren, B. (2022). "Language of Instruction in Education in Africa: How New Questions Help Generate New Answers." *International Journal of Educational Development*. Juz. 88 (1) DOI: <https://doi.org/10.1016/j.ijedudev.2021.102524>.
- Vernet, T. (2009). "Slave Trade and Slavery on the Swahili Coast (1500-1750)". In B.A. Mirzai, I.M. Montana et P. Lovejoy. *Slavery, Islam and Diaspora*, Africa World Press, 37-76.
- Vilhanová, V.P. (2007). "Christian Missions in Africa and Their Role in The Transformation of African Societies." *Katika Asian and African Studies*, Juz. 16, (2), 249-260.
- Wahab, E. O; Odunsi, S.O. and Ajiboye, O.E. (2012). "Causes and Consequences of Rapid Erosion of Cultural Values in a Traditional African Society." *Journal of Anthropology*. Juz. 2012, Article ID 327061, <https://doi.org/doi:10.1155/2012/32706>.
- wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Heinemann.
- Wizara ya Habari Huduma ya taifa ya Habari, (1985) AFRICA: A Century After its Division in the Berlin Conference, 1885. Mkondoni <http://archives.au.int/handle/123456789/5936>.
- Wynter, S. (2003). Unsettling the Coloniality of Being/power/truth/freedom: Towards the Human, after Man, its Overrepresentation—An Argument. *CR: The New Centennial Review*, 3(3), 257–337.